**OFISI YA RAIS - TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA WILAYA KILOLO**
SHULE YA SEKONDARI UHAMBINGETO

S.L.P 190
**MAZOMBE**
IRINGA

☎ +255 764 444 001 /0626921106
0753697455
**Email:** malenga29@gmail.com

**KUMB NA:UHSS/KDC/IRA/DES/2020/1** **Tarehe:** 15/12/2020

**JINA LA MWANAFUNZI……………………………………………………**

KIJIJI**: ……………………………** SHULE YA MSINGI ALIYOSOMA**: …………………………..**

---

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA SEKONDARI UHAMBINGETO MWAKA 2021**

Ninafurahi kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari Uhambingeto kwa mwaka 2021. Unatakiwa kuripoti shuleni **tarehe 11/01/2021** siku ya **Jumatatu saa moja kamili asubuhi ukiwa na mzazi/mlezi wako.**

1. **MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

Serikali inagharamia elimu hivyo mwanafunzi atasoma bila mzazi kulipa ada isipokuwa kama kuna mchango wa fedha ambao wazazi kupitia vikao na kamati / bodi ya shule iliridhia kwa pamoja. Aidha, wajibu wa mzazi ni kununua sare za shule, Vifaa vya kujifunzia kama madaftari, kalamu, kugharamia chakula kwa wanafunzi wa kutwa na hostel (daharia) na matibabu.

**SARE YA SHULE**

**A. WAVULANA**

a) Suruali mbili (02) za rangi ya kijani kibichi zenye marinda mawili kila upande. Suruali **isiwe** ya kubana (modo) chini na juu.
b) Shati mbili (2) rangi nyeupe tetron za mikono mirefu.
c) Tai mbili (2) rangi ya kijani kibichi.
d) Viatu vyeusi vya kamba jozi mbili (02) ( vyenye visigino vifupi )
e) Sweta zenye rangi ya Zambarau (02)
f) Soksi nyeusi jozi mbili (02)
g) Track Suit rangi ya bluu na Raba jozi moja (1) kwa ajili ya michezo.

**B. WASICHANA**

a) Shati mbili (2) tetroni rangi nyeupe ya mikono mirefu.
b) Sketi mbili za kijani kibichi linda box, malinda nane. Sketi iwe **ndefu** kuvuka magoti.
c) Viatu vyeusi vya kamba jozi mbili (2) vyenye visigino vifupi
d) Sweta zenye rangi ya Zambarau mbili (02)
e) Track Suit rangi ya bluu na Raba jozi moja (1) kwa ajili ya michezo.
f) Soksi nyeupe jozi mbili (2)

**C. KWA WASICHANA WA KIISLAMU**

a) Suruali jozi mbili (02) rangi ya kijani kibichi isiyo bana /Sketi ndefu inayovuka magoti.
b) Hijabu nyeupe mbili (02)
c) Shati za tetroni nyeupe nusu kanzu mbili (02) zenye mikono mirefu, ziwe pana na **zisizoangaza.**

**D. MAHITAJI BINAFSI YA MWANAFUNZI (KITAALUMA)**

Mwanafunzi anapokuja kuanza kidato cha kwanza aje na mahitaji yafuatayo atakayotumia darasani.

i. Daftari kubwa 10 (counter book, 2 quire)) kwa kuanzia.
ii. Rula, peseli na karamu za wino za kutosha.
iii. Mkebe (Mathematical set) 01
iv. Kamusi (Dictionary) ya Kiingereza moja (01)

**E. MAHITAJI MENGINE YA SHULE**

i. Bunda moja (01) la karatasi A4 ***(Duplicating Ream Paper A4)*** kwa ajili ya kudurufia mitihani na kufanyia mazoezi darasani. Siku unayoripoti shuleni utaikabidhi ofisi ya Mkuu wa Shule.
ii. Ufagio wako wa kufanyia usafi kwenye mazingira ya shule, wakati wote utautunza mwenyewe.

**NB: FOMU/ VITU MUHIMU ANAVYOTAKIWA KUJA NAVYO WAKATI WA KURIPOTI NI:**

i. FOMU YA AFYA (Medical Examination Form) – Imeambatanishwa.
ii. KIVULI CHA CHETI CHA KUZALIWA (Photocopy).

Nakutakia maandalizi mema,

**MALENGA M. LUKUVI**
**MKUU WA SHULE**

## SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu na.25 ya mwaka 1978 na inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi yenye dhamana ya Elimu, pamoja na Ofisi ya Rais - TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi na Uendeshaji wa masuala ya Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo muhimu yafuatayo:

a) Mahudhurio
   Kuthamini muda wa kuwepo mahali unapotakiwa kwa mujibu wa ratiba au maelekezo kutoka Uongozi wa Shule.
   i. Kuwahi kufika shuleni na kuwa mstarini saa **12.30 (saa kumi na mbili na nusu) asubuhi** kila siku za masomo
   ii. Kuhudhuria shuleni kwa muda wote wa masomo kwa siku zote
   iii. Kuhudhuria kazi zote za mikono
   iv. Kuhudhuria mikutano ya shule **mfano** Baraza la shule,Ukaguzi wa usafi, kupandisha Bendera ya Taifa,Maandamano, vikao vya Madarasa,Masomo ya Dini n.k.
   v. Kuitika miito ya dharura mara moja
b) Kuwathamini na kuwaheshimu wanafunzi wenzako wote wakubwa kwa wadogo
c) Kusimama na kusalimu Mwalimu au mtu yeyote anayekuzidi umri anapopita au kuingia mahali ulipo na kupokea mizigo ni lazima.
d) Ni wajibu wako mwanafunzi Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote, kutii kengele na Kuwahi kila mahali utakapohitajiwa na kwa wakati.
e) Kutumia lugha nzuri wakati wote unapokuwa shuleni na hata nyumbani
f) Kuthamini na kuheshimu kazi za aina zote
g) Kushirikiana na kusaidiana na wanafunzi wengine katika kazi
h) Kuitika wito mara moja kukimbilia aliko anayekuita
i) Kuheshimu bendera ya Taifa, Picha za viongozi wa vyama, serikali na Nembo ya Taifa, Wimbo wa Taifa, wimbo wa shule na fedha za Taifa
j) Kuheshimu vikao ,Ofisi za shule mali binafsi na za umma
k) Kukaa kimya darasani na mahala pengine popote penye mkusanyiko.
l) Kutoka nje kwa ruhusa ya mwalimu au kiongozi wa darasa
m) Huruhusiwi kutumia madawa ya kulevya kama pombe au sigala ndani na nje ya shule
n) Kuwa mfano mzuri wa kuigwa (kitabia) uwapo ndani na nje ya shule
o) Si ruhusa kugombana, au kutukana, au kupigana
p) Huruhusiwi kushiriki uasherati (uzinzi), Wizi na utapeli
q) Huruhusiwi kutoka nje ya mipaka ya shule bila kibali maalum baada ya kufika shuleni.Kibali maalumu cha ruhusa kitatolewa na mwalimu wa zamu au mwalimu wa Darasa au mwalimu wa malezi.
r) Usitembelee maeneo yafuatayo bila ruhusa toka kwa mwalimu
   i. Ofisi za shule
   ii. Maabara
   iii. Nyumba za wafanyakazi / walimu

s) Hurusiwi kabisa kutembelea maeneo yafuatayo ukiwa ni mwanafunzi ama ikiwa ni mida ya darasani au ukiwa nyumbani siku za wikiendi.
    i. Vilabu vya pombe au bar *(Sehemu zote zinazouza vileo)*
    ii. Majumba ya kufikia wageni. *(Guest House/ Lodge)*
    iii. Majumba ya starehe kama vile majumba ya disco au klabu.
    iv. Nyumba za kuoneshea mpira au kucheza michezo ya video.
    v. Sehemu wanazokodisha mikanda ya video. *(Studio)*

**UTARATIBU WA UVAAJI SARE YA SHULE**

i. Unapaswa kuwa na sare ya shule zinazokubalika na kwa wakati kama utakavyopangiwa kwa:
    a) Wakati wa masomo
    b) Safari za nje ya shule kwa jina la shule
    c) Wakati wa maandamano
    d) Kuwa na Nguo za Michezo na vazi la kazi za mikono

ii. Ni marufuku mwanafunzi kuvaa viatu vyenye kisigino kirefu, soli ndefu au pana wala kiatu kilichochongoka mbele, mkanda usio mweusi, mkanda wa nguo/kitambaa, mapambo mengine kama heleni, mikufu, bangili hayaruhusiwi.. Pia ni ***marufuku kufuga rasta, nywele ndefu, ndevu, kupaka kucha rangi, kupaka wanja, kupaka piko, kujichubua, kunyoa kipara au kiduku.*** Atakayepatikana na makosa haya atarudishwa nyumbani na kumwita mzazi ama kufukuzwa shule kabisa.

**MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE:**

a) Wizi
b) Utoro
c) Ulevi wa aina yeyote
d) Uvutaji au uuzaji wa bangi, sigara, mirungi, kubeli na mihadharati mingine.
e) Kosa la jinai
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
g) Kuoa au kuolewa
h) Kupata au kusababisha mimba.
i) Kutoa au kushawishi kutoa mimba.
j) Kugoma, kuchochea au kusababisha mgomo
k) Uzinzi,Ushoga , usagaji, na ubakaji au ulawiti
l) Kupiga au kupigana
m) Kudharau Bendera , Nembo, fedha, Wimbo na Viongozi wa kitaifa
n) Kumiliki simu ya Mkononi
o) Kugomea/ kukataa adhabu kwa makusudi
p) Makosa mengne yafananayo na hayo hapo juu.

**WAGONJWA**

Mwanafunzi atakapougua atapata kibali cha kwenda kutibiwa kutoka kwa Mwalimu wa zamu au Mwalimu wa darasa au mwalimu mlezi.Shule haitoi huduma za afya , hivyo mzazi atawajibika kutoa gharama za matibabu za mwanae pindi atakapougua akiwa kwenye mazingira ya shule na iwapo atafikishwa kwenye vituo vya kutolea huduma (Zahanati) na uongozi wa shule.

**USAFI**

Utawajibika kushughulikia

i. Usafi wako binafsi (Mwili na mavazi)
ii. Usafi wa maeneo ya shule utakayopangiwa na mwalimu wa zamu au kiranja

**UTORO**

Mwanafunzi ambaye hatahudhuria shuleni bila taarifa atahesabiwa kuwa ni mtoro. Taarifa ya kutohudhuria shuleni iwasilishwe shuleni siku hiyo ya matatizo kwa Mwalimu wa zamu au Mwalimu wa darasa.

**MWISHO**

Tafadhari hakikisha umesoma kwa makini na kuzielewa sheria zilizoainishwa hapo juu ili uweze kuishi kwa furaha na amani hapa shuleni.

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MINISTRY OF EDUCATION AND VOCATIONAL TRAINING**
**UHAMBINGETO SECONDARY SCHOOL**

# MEDICAL EXAMINATION FORM

(To be completed by a Medical Officer in respect of all form ones students)

---

**Student's full name……………………………………………………………………………………..**

**Age ……………  Year …………………  Sex …………………….**

- **Blood count (Read and white)…………………………………………………………………**
- **Stool Examination……………………………………………………………………………..**
- **Syphilis and other venereal Diseases Test……………………………………………………..**
- **T.B. …………………………………………………………………………………………………**
- **Eye Test…………………………………………………..……………………………………..**
- **Ears ………………………………………………………..…………………………..……**
- **Spleen…………………………………………………………..……………………………………**
- **Abdomen ……………………………………………………………………………………**
- **Urine for protein test………………………………………………………………………………**
- **Test of pregnancy (For girls only)…………………..…………………………………………**

Additional information (If any) e.g. physical defects impairment Infections chronic or family diseases etc

**……………………………………………………………………………………………………………..**
**……………………………………………………………………………………………………………..**
**……………………………………………………………………………………………………………..**

I certify that the above is fit /unfit to pursue his/her lessons /duties as required.

**Station ……………………………………………  Signature…………………….……………………….**

**Date…….…………………………… Designation……………………………………….…………**

**<u>Note: Medical Officer</u>**

*At the time of examination please treat the individual for anything you note for pupils /employee. This completed form should be sent to the school with your acceptance form brought when you come to school. No student can be enrolled without this certification physical fitness..*

---